

Rafiki yangu, utakuwepo hapo? Bado hujaokoka, na bado hutishiki? Na kama ni hivyo, kwa nini hutachukua tahadhari leo, sasa hivi, kabla ya kuchelewa milele? Unajua ya kuwa utahukumiwa? Neno la Mungu liko wazi kabisa. Linasema: “Basi ni hivyo, kila mtu miongoni mwetu atatoa habari zake mwenyewe mbele za Mungu” (Rum 14:12). Hakuna atakayejitokeza badala yako, au wewe uhukumiwe kwa dhambi za mtu mwingine. Lazima utajibu kwa ajili yako mwenyewe. Na usipookoka, lazima utakuwepo hapo.

Nani atakuwa hakimu? Yesu Kristo mwenyewe, Yeye anayetamani kuwa Mwokozi wako. Sikiliza Neno tena: “Tena Baba hamhukumu mtu yeyote; bali amempa Mwana hukumu yote” (Yoh 5:22).

Mhalifu alikuwa karibu agongwe na gari, wakati mtu alipotokea ghafla na kumwokoa. Baadaye aliposimama kizimbani, akishtakiwa kwa uovu mkubwa. Hakimu alikuwa ni yule aliyemwokoa katika ile ajali ya gari.

Yule mhalifu akamsihi, akitegemea labda atamwokoa tena kama alivyofanya kabla. “Siku ile” hakimu alieleza, “nilikuwa mwokozi wako; leo mimi ni hakimu”. Na alifungwa.

Mungu ametoa wakati fulani na inawezekana ni sasa kwamba unaweza kumfanya Yesu Kristo kuwa Bwana wa mabwana na Mfalme wa wafalme wako. Je, itakuwa sasa au baadaye? Sasa kwa hiari yako mwenyewe, au baadaye kwa lazima? Je, utampokea sasa kama Mwokozi, au baadaye kama hakimu? Lazima iwe moja kati ya hayo. Je ni yepi kwako? Rafiki yangu, nakushihi umpokee yeye, na umpokee SASA.

Na Oswald J. Smith



**Revival**  
MOVEMENT ASSOCIATION

Tuma kwa:


**Revival Movement Association**  
10 Kinallen Road, Dromara,  
Dromore, BT25 2NL, Northern Ireland  
[www.revivalmovement.org](http://www.revivalmovement.org)

God's JUDGEMENT DAY - Swahili

# SIKU ya HUKUMU ya MUNGU



# SIKU ya HUKUMU ya MUNGU



Hukumu ya Kiti cheupe cha Mungu iko tayari. Hakimu ameketi. Malaika na malaika wakuu wamehudhuria. Wote walioko mbinguni wamekusanyika. Mamilioni yasiyohesabika, wakiwa kwenye mshangao mkuu, wanaangalia tukio hili la kutisha. Kukiwa na hofu katika kila uso wanangoja. Tukio la mwisho wa wakati linatokea. Hakuna kitu kingine kinachokuwa muhimu tena. Kila kitu kingine katika hali ya maumbile imeshapita. Ni siku ya hukumu ya Mwenyezi Mungu. Katika ukimya huo wa ajabu, wafu wanatokea; wenye dhambi wakubwa na wadogo, kutoka kila taifa, jamaa,

wenye dhambi nyingi, wauaji, wachawi, waongo, wezi, waabudu sanamu, wazinzi, walevi, watukanaji, wadhalimu wanafiki, wanaoivunja siku ya Bwana, wasioamini, na wahalifu wakubwa pamoja na wale waliompuuza na kumsahau Mungu.

Kutoka katika viwanja vikubwa vya vita duniani ambapo mavumbi yao yamekuwepo kwa mamia ya miaka, watakuja; kutoka katika vilindi vya bahari ambapo meli zilizama karne nyingi zilizopita; kutoka makaburini, tangu yaliposahauliwa, watakuja. Oh! Ni mkutano wa namna gani! Na jinsi wanavyoendelea kuja, milioni juu ya milioni, hawa walikuwa wanaume na wanawake duniani – wote wanatakiwa kuonekana mbele za Mungu, kutoa hesabu kwake ambaye walimpuuza na kumdharau. Watatazama njia hii na ile, wakitafuta njia ya kukwepa. Wataiita milima iwaangukie, na kuwaficha kutoka kwa yeye aketiye juu ya kiti cha enzi. Lakini hakuna njia ya kukwepa, hakuna msaada. Ni siku ya maangamizi yao.

Na vitabu vitafunguliwa, vitabu vilivyojaa kumbukumbu ya maisha yao duniani. Kila dhambi imewekwa katika kumbukumbu, kila kosa limeandikwa, kila kushindwa

na nafasi ya kufaa iliyopotezwa imeandikwa. Matendo ya zamani yaliyosahaulika, vitu viovu vilivyofichwa kwa makini kutoka katika kila jicho la mwanadamu, yote - ndiyo, sasa yote yanawekwa wazi, na ulimwengu wote unasikiliza juu ya kufunuliwa kwa mambo hayo ya aibu. Kwa fadhaa wanasimama, wakiwa wamejawa hofu, wanangojea, pasipo kusema kitu wanasikiliza. Mwishoni kitabu cha uzima kinaletwa. “Na iwapo mtu yeyote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto” (Ufu 20:15). Hapa sasa sio swali kuhusu wingi wa dhambi zao, kwa sababu wote wana hatia. Ni hitaji moja tu, ni wazo moja tu:

**“Je, jina langu limeandikwa pale Katika ukurasa mweupe na safi Katika Kitabu cha Ufalme Wako? Je, jina langu limeandikwa pale?”**

Bure tu watatafuta, watachunguza kurasa zake! Nafasi yao ya mwisho imekwisha pita, tumaini lao la mwisho limekwisha.

**“Na, oh! Kutakuwa na kilio na kuomboleza kwa jinsi gani, Wakati waliopotea watakapoelezwa hali yao Wamelilia miamba na milima, Wameomba, lakini maombi yao yamechelewa mno.”**